**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

18 APRILI, 2017

# YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 3
2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 ........................................................ 5
2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa ............... 5
2.1.1 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund....... 6
2.1.2 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ...................... 7
2.1.3 Mradi Na. 6576 - Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)........... 8
2.1.4 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)..................................... 9
2.2 Matokeo ya Ukaguzi........................................................................ 9
2.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini "Support to Tanzania Social Action Fund" ................................................................ 10
2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)......................................................... 13
2.2.3 Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF). .................................. 16
2.2.4 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).................................... 17
2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 .......................................................... 19
3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 ............. 21
3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ........................................................... 21
3.1.1 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.................................... 22
3.1.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ....... 25
4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ...................................................... 26
4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 26
4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2017/2018....................... 29
5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI............................................................ 33
6.0 HITIMISHO ......................................................................................... 36

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yalipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uchambuzi wa Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya

Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Baada ya kutimiza sharti hilo, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya ofisi hii kwa mwaka 2016/17 na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya Mafungu Tisa (9) yafuatao:-

i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;
iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma;
viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; na
ix) **Fungu 11:** Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa baada ya uchambuzi wa Taarifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii yaliyowasilishwa, Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi hii inajikita katika maeneo manne yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ilitengewa **Tsh. 466, 217, 858, 000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupitia Mafungu Manne kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – Tshs. 430,449,029,000/=

ii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma – **Tshs .7,550,000,000/=**

iii) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 1,000,000,000/=**

iv) **Fungu 6**: Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi - Tshs**. 27,218,829,000/=**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia sharti la kipindi kisichozidi siku Saba (7) ambalo limewekwa na Kanuni, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi hiyo, inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi **416,362,198,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Katika utekelezaji wake, Mradi huu umefikia Awamu ya Tatu, inayojikita katika kusaidia jamii ya Watanzania kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii, pamoja na kuhamasisha utawala bora na uwajibikaji.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, hadi sasa takribani Watanzania milioni 5.9 wameandikishwa ili kunufaika na Mpango huu ambao umesaidia sana kaya maskini kuboresha

maisha kwa kumudu kupata chakula, kuwezesha Watoto kuhudhuria shuleni pamoja na Kliniki kwa wale walio chini ya umri wa miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa zaidi kuwa kwa familia zenye Watoto wanaopaswa kupata huduma ya elimu na afya, mahudhurio ya shuleni na kliniki, vimekuwa vigezo vikuu vya kuzingatiwa ili walengwa waendelee kunufaika na utaratibu wa kupokea fedha. Sababu ya vigezo hivyo ilitajwa kuwa ni kutokana na Watoto kutoka Kaya maskini nchini kuwa waathirika wakubwa wa kukosa huduma za elimu na afya.

Ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Mikoa Mitano nchini. Mikoa hiyo ni Morogoro, Tanga, Mbeya, Njombe na Iringa.

### 2.1.2 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 2,000,000, 000/=** na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 kiitwacho *"Policy and Planning"* cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mpango huu unaandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa

umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria nchini, na kwa mantiki hiyo kuwasaidia Wanyonge kurasimisha mali walizonazo (ardhi na biashara) ili ziwawezeshe kujikwamua kiuchumi.

Kwa mujibu wa Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, mpango huu umekuwa ukihamasisha na kuchangia ujenzi wa Masijala ya Ardhi katika Vijiji/Mitaa, kwa ajili ya uhifadhi madhubuti na salama wa nyaraka (Hati za Hakimiliki za Kimila na nyaraka nyingine) pamoja na matumizi mengine ya Serikali za Vijiji au Mitaa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea jumla ya maeneo Kumi na Moja (11) yaliyoko katika Mikoa Minne (4) ambayo ni Njombe, Morogoro, Dodoma na Mbeya kwa lengo la kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji.

### 2.1.3 Mradi Na. 6576 - Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa shughuli za mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 500, 000, 000/=** chini ya Kifungu 1003 kiitwacho "*Policy and Planning*" cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Taarifa ziliainisha

majukumu ya msingi katika Mradi huo ambayo ni kutoa mikopo, ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati, katika sehemu mbalimbali nchini. Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi huu katika Mikoa miwili ya Njombe na Morogoro, kwa kutembelea jumla ya Vikundi Sita (6).

#### 2.1.4 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** chuo hiki kilianzishwa ili kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala, kutoa ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti na kutoa machapisho ya kitaalam katika utumishi wa Umma. Kamati ilijulishwa kuwa, chuo hiki kinazo jumla ya Kampasi Sita (6) katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kamati ilitembelea kampasi mbili kati ya sita sawa na asilimia 33.3% ya idadi ya kampasi za chuo hicho. Kampasi zilizotembelewa ni za Mbeya na Tanga.

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini "Support to Tanzania Social Action Fund"

**Mheshimiwa Spika**, katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Mikoa Mitano ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, mambo kadhaa yalibainika kuhusiana na utekelezaji huo, ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 01** linafafanua zaidi kuhusu hali ya Mradi huu.

**Jedwali Na. 01:** Hali ya Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Maskini katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati

| Mkoa | Mtaa (M) Kijiji (K) | Awamu za Malipo | Fedha iliyolipwa katika Awamu zote | Kaya nufaika | Kaya zilizoondolewa | % ya Kaya zilizoondolewa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Morogoro | Kilongo (M) | 11 | 50,066,699 | 106 | 13 | 10.92 |
| Tanga | Makuyuni (K) | 10 | 39,179,000 | 115 | 7 | 5.73 |
| Mbeya | Lumbila (M) | 10 | 27,600,000 | 71 | 0 | 0 |
| Iringa | Mlanda (K) | 10 | 31,372,000 | 86 | 3 | 3.48 |
| Iringa | Isakalilo (M) | 11 | 17,016,000 | 236 | 55 | 18.90 |
| Njombe | Uwemba (K) | 11 | 51,676,000 | 139 | 0 | 0 |

**Chanzo:** Taarifa za TASAF kuhusu Mpango za Ruzuku kwa Kaya Maskini nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza. Kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**a) Mafanikio;**

i) Malipo yamefanyika kwa wastani wa Awamu 11 hadi Februari, 2017 ambapo jumla ya Shilingi Milioni 216 zimelipwa katika kipindi hicho;

ii) Mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mpango;

iii) Walengwa wa mpango wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, kilimo, ufugaji na biashara;

iv) Watoto wa Walengwa wanapata mahitaji ya shule na hivyo kuhudhuria shuleni kikamilifu na Kliniki kwa walio chini ya umri wa miaka mitano; na

v) Walengwa wengi wamewezeshwa kujiunga na Bima ya Afya ya Jamii (CHF).

**b) Changamoto;**

i) Bajeti finyu ya mpango ikilinganishwa na idadi ya Kaya maskini;

ii) Malalamiko ya uonevu kutoka kwa Walengwa walioondolewa katika mpango kwa madai ya kukosa sifa. Mfano, Kaya Tatu katika Kijiji cha Mlanda, Mkoani Iringa, zimekata rufaa katika ngazi ya Wilaya kupinga kuondolewa katika mpango;

iii) Zipo Kaya maskini nyingi hazijaingizwa katika Mpango wa ruzuku;

iv) Sehemu kubwa ya walengwa ni Wazee hivyo hutumia ruzuku wanayopata kwa ajili ya mlo tu, kwani hawana nguvu za kujishughulisha na uzalishaji;

v) Walengwa wa mpango waliojiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kukosa huduma ya afya katika Zahanati binafsi kwani haziko tayari kuwahudumia wateja wenye aina hiyo ya bima;

vi) Ukosefu wa Zahanati au Vituo vya Afya, unakwamisha baadhi ya Walengwa kutimiza masharti ya afya (kupeleka Kliniki Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano).

### 2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika,** katika maeneo Kumi na Moja (11) ya Mikoa Minne 94) ambayo Kamati iliyatembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 02** linatoa muhtasari wa hali utekelezaji wa mpamgu huo.

**Jedwali Na. 02:** Hali ya utekelezaji wa MKURABITA katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati

| Mkoa | Mtaa (M) Kijiji (K) | Urasimishaji Ardhi/Biashara | Fedha iliyotumika (Tsh) | Hati Miliki zilizoandaliwa | Hati Miliki zilizochukuliwa | % ya Hati zilizochukuliwa na Wananchi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Morogoro | • Tuelewane<br>• Kihonda (B) | Viwanja 822 | - | 822 | 132 | 16.05 |
| Njombe | • Joshoni (M)<br>• Melinze (M)<br>• Mpechi (M)<br>• Nazareti (M)<br>• Idundilaga (M) | Viwanja 1003 | Milioni 62 | 650 | 602 | 92.61 |
| Njombe | Kambarage (M) | Wiwanja 632 | Milioni 34 | 80 | 10 | 12.5 |
| Dodoma | Pwaga (K) | Mashamb a 1,277 | - | 1,031 | 1,031 | 100 |
| Dodoma | Pwaga (K) | Masijala ya Ardhi | Milioni 32 | - | - | - |

**Chanzo:** Taarifa za MKURABITA kuhusu urasimishaji wa ardhi na biashara.

## a) Mafanikio

i) Baadhi ya Wananchi wamekuza mitaji ya biashara zao kutokana na mikopo waliyoipata kwa kutumia Hati Miliki za Kimila kama dhamana. Mfano; Wanufaika wanne (4)

katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, wamekopa kati ya Shilingi Milioni 50 hadi 500;

ii) Mpangilio mzuri wa maeneo, na hivyo kuepusha au kuondoa migogoro katika maeneo yaliyopimwa na kurasimishwa;

iii) Kuongezeka thamani kwa maeneo yaliyorasimishwa;

iv) Wanawake kumilikishwa Hati Miliki za ardhi peke yao au pamoja na Wenza wao;

a) **Changamoto;**

i) Bajeti ndogo ya MKURABITA inaathiri utekelezaji wa mpango huu;

ii) Baadhi ya Wananchi kushindwa kugomboa Hati za Miliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa; Mfano, katika maeneo yaliyotembelewa mkoani Morogoro kati ya Hati 822 zilizoandaliwa ni 132 tu (sawa na asilimia 16.05) ndiyo zimechukuliwa na Wananchi;

iii) Wafanyabiashara wengi kukosa mwamko wa kurasimisha biashara zao;

iv) Baadhi ya Taasisi za fedha haziko tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Hati za Hakimiliki za Kimila;

### 2.2.3 Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF).

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mradi huu, katika vikundi Sita (6) ambavyo Kamati ilitembelea kwenye Mikoa ya Morogoro na Njombe, mambo kadhaa yalijiri yakijumuisha mafanikio na changamoto. Ufafanuzi zaidi unatolewa kupitia **Jedwali Na. 03**

**Jedwali Na. 03:** Mikoa na Vikundi vilivyokopeshwa fedha na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

| Mkoa | Jina la Kikundi | Shughuli ya Kikundi | Thamani ya Mkopo | Muda wa Mkopo |
|---|---|---|---|---|
| Njombe | Vijana Gaurage | Uchomeleaji (Welding) | Milioni 2.5 | Miezi 6 |
| Njombe | Upendo | Ukamuaji wa Mafuta ya Alizeti | Milioni 2.5 | Miezi 6 |
| Njombe | Women Handcraft Group | Ufumaji | Milioni 2.4 | Miezi 6 |
| Njombe | Lumumba Group | Ufugaji Nguruwe, Ng'ombe & Kuku | Milioni 2.5 | Miezi 6 |
| Morogoro | Mwale Cleaners | Uzoaji Taka | Milioni 10 | Miezi 6 |
| Morogoro | Women Bakery Group | Uokaji Mikate | Milioni 5 | Miezi 6 |

**Chanzo:** Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

a) **Mafanikio**

i) Vikundi vya Vijana (2) na Wanawake (14) vimepata mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mikopo bila kuwa na dhamana;

ii) Vijana na Wanawake wajasiriamali wamewezeshwa kujiajiri; na

iii) Makundi Maalum ya Walemavu yamepatiwa mikopo. Mfano; Watu wenye Ulemavu 16 pamoja na Wanaoishi na VVU wamekopeshwa **Shilingi Milioni Saba (7)** Mkoani Morogoro.

b) **Changamoto;**

i) Bajeti ndogo ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) hivyo kushindwa kufikia walengwa wengi;

ii) Mtandao (Network) mdogo wa shughuli za Mfuko nchini; na

iii) Shughuli za Mfuko zimejikita zaidi maeneo ya mjini, jambo linalowanyima fursa ya mikopo Wananchi wa vijijini.

### 2.2.4 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza utendaji wa Chuo hiki kwani kimekuwa nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma, hasa kwa

kuzingatia ukweli kwamba, hakuna Taasisi nyingine yenye jukumu la kutoa mafunzo hayo. Katika ziara yake, kwenye Kampasi ya Mbeya kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Majengo yanayotumiwa ni ya kukodi kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya, jambo linalokigharimu chuo S**hilingi Milioni 22** kwa Mwezi, sawa na **Shilingi Milioni 264** kwa Mwaka. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ilizopata Kamati kuna mazungumzo yanayoendelea baina ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhusu uwezekano wa chuo kumilikishwa majengo hayo;

ii) Pamoja na kukosa majengo yake, Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Mbeya kimeendelea kufanya vizuri katika kutimiza malengo yake, kwa kutoa Mafunzo na ushauri wa kitaalamu katika Utumishi wa Umma; na

iii) Bado chuo kinatumia Walimu wa Mkataba badala ya kuwa na Watumishi wa ajira za kudumu;

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

i) Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ungeweza kufanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zingetumika kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za Wafadhili. Tangu kuanza kwa mpango huu katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia **Shilingi bilioni 3.6** kati ya **Shilingi bilioni 60.5** ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **5.9** ya kiasi kilichotakiwa;

ii) Itikadi za kisiasa walizonazo Viongozi na Watendaji zinaweza kusababisha mgawanyiko miongoni mwa Wananchi na hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini;

iii) Uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa Walengwa wa Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini kuchukua fedha zao wenyewe utasaidia kufanikisha utekelezaji wa mpango na kufikiwa kwa lengo la kutoa elimu ya afya kwa walengwa;

iv) Kwa kuwa Wazee walio katika Vituo vya kulelea Wazee nchini wanakidhi sifa na vigezo vya kusaidiwa, ni jambo jema kutekeleza mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini

katika vituo hivyo na kwamba utekelezaji huo utasaidia wazee hao kumudu maisha;

v) Dhamira ya kuwataka Wanufaika wa Mpango wa Ruzuku kwa kaya maskini wajiunge na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) itafanikiwa zaidi iwapo Serikali itawezesha Zahanati binafsi kutoa huduma kwa walengwa hao;

vi) Uendeshaji wa Zoezi la kuhakiki na kuziondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ni muhimu na utakuwa na tija zoezi hilo likifanyika kwa kuzingatia taratibu na kwa haki ili kuepusha kuibuka kwa malalamiko kuhusu uonevu na kutotendewa haki kwa baadhi ya waliokuwa wanufaika.

vii) Uhaba wa fedha unachangia kukwamisha Zoezi la kupima na kurasimisha ardhi na biashara za Wananchi linalotekelezwa na MKURABITA.

viii) Halmashauri zikishirikiana na MKURABITA, zinaweza kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi, na kuwezesha Wananchi kutumia Hati za Haki Miliki wanazopata kama dhamana ya mikopo kutoka taasisi za fedha.

ix) Uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa Wanufaika wa MKURABITA kulipia na kuchukua Hati Miliki za Kimila kwa wakati, ni jambo muhimu katika kufanikisha ukusanyaji

wa fedha na kuendeleza zoezi hilo katika maeneo mengine;

x) Huduma ya mikopo kwa Vijana na Wanawake kutoka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, itafanikiwa zaidi iwapo mfuko huo utawezeshwa kifedha na kufungua matawi maeneo mengine ya nchi;

xi) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kitamilikishwa majengo kinayoyatumia kwa ajili ya Kampasi ya Mbeya, hatua hiyo itasaidia kuepusha gharama kubwa za pango zinazolipwa kila mwaka;

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa

kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

### 3.1.1 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa:-

i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa katika mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan); na

ii) Fedha zinazotolewa kutoka Hazina hazipatikana kwa wakati jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa Mpango kazi wa kuyaendea malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (na mafungu yake) kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari (katikati ya robo ya Tatu ya mwaka wa fedha

2016/17) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi zaidi unabainisha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea Shilingi **527, 116, 217, 512/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia **59.75** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/2017 na mwaka 2015/2016 na kubaini kuwa Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa asilimia **23. 11** ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16 ambapo upatikanaji wa fedha ulikuwa ni sawa na asilimia **82. 86** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa mwaka huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebainisha kwamba, hadi kufikia Mwezi Februari, 2017, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

na Mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **246, 780, 369, 584/=** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na Asilimia **52. 93** ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

Kiasi kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa asilimia **21.28** ikilinganishwa na kiasi kilichokuwa kimepatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni sawa na asilimia **74.21** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa mwaka huo.

Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha (ie. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa ujumla haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani Asilimia **59.75** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Tafsiri inayoweza kuelezwa hapa ni kwamba, kiwango kilichokadriwa kwa ajili ya kila robo ya mwaka wa fedha hakikupatikana, kwani ilitakiwa katika kipindi hicho upatikanaji wa fedha uwe zaidi ya Asilimia **70** ya fedha iliyoidhinishwa.

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya fedha ya Matumizi ya Kawaida Shilingi **280,335,847,928/=** ilikuwa imepokelewa kiasi ambacho ni sawa na Asilimia **67.41** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hii inaonesha kwamba, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilikuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo zilizopatikana katika kipindi kama hicho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha umeendelea kudorora ikilinganishwa na miaka iliyopita na bado ile kasumba ya kwamba, fedha za matumizi

ya kawaida ni lazima ziwe juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo imeendelea kutamalaki.

### 3.1.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Rais - Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo Tisa (9) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Rais Menejementi ya Utumishi wa Umma, na Utawala Bora, iliweza kuzingatia kikamilifu maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya Maoni na ushauri uliozingatiwa ni kuhusu:-

i) Uhakiki wa Watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa mshahara ili kuepusha upotevu wa fedha za Umma, ambapo katika kipindi cha Machi hadi Agosti, 2016 jumla ya **Watumishi hewa 19,708** walibainika na kuondolewa katika Mfumo wa Mshahara; na

ii) Tathmini kwa lengo la kubaini Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini wasio na sifa, na kuwaondoa katika utaratibu huo, ambapo hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya Kaya za **Walengwa 63,819** zilikuwa zimebainika na kuondolewa katika utaratibu huu kutakana na sababu mbalimbali.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Tisa (20; 30; 32; 33; 67; 94; 04 na 11) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo **186** na baadhi ya hayo ni malengo yafuatayo:-

i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake, pamoja na ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;

ii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha

Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;

iii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutakatisha mali zilizopatikana kwa njia ya Rushwa na Ufisadi;

iv) Kutumia Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kuunganisha Taasisi za Serikali 80 kwenye mfumo wa pamoja na salama wa barua Pepe wa Serikali ili kufikisha taasisi 281 zinazotumia mfumo;

v) Kuanzisha mchakato wa kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya raslimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao (*online application*) baada ya kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (Ethics Management Information System - EMIS).

vi) Kuandaa taarifa za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha; na kutafiti namna ya kutoa motisha kwa kuzingatia utendaji katika Utumishi wa Umma, na

vii) Kuendelea kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma 25 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu, Dodoma; na kuimarisha Mfumo wa

Kielektroniki wa Masijala (e-Filing) ili kuboresha huduma na kurahisisha zoezi la Serikali kuhamia Dodoma;

viii) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Baraza la Mawaziri katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi;

**Mheshimiwa Spika,** ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 821,322,347,674.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 430,351,457,674** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kaiwada, na **Shilingi 390,970,890,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 23,214,791,000 (**sawa na asilimia 5.39**)** ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 407,136,666,674** (sawa na asilimia 94.61) ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa katika mwaka ujao wa fedha imepungua kwa **Shilingi 60,788,585,326 (**sawa na **asilimia 6.89)** ikilinganishwa bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2016/17 ambayo ilikuwa **Shilingi 882, 110, 933, 000.**

Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, kiasi kinachoombwa kuidhinishwa kimepungua kwa **shilingi 75,246,968,000** (sawa na **asilimia 16.13)** ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 466,217,858,000** kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

## 4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kufanya ulinganisho na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uchambuzi wa Kamati ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la Bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Mambo yaliyobainika ni haya yafuatayo:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/18 ambayo ni **shilingi bilioni 821** ni sawa na **asilimia 2.59** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa

Mpango wa Maendeleo wa 2017/18 ni **shilingi bilioni 31,699;**

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/18 unaonesha ongezeko la bajeti kwa **asilimia 7.31**, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2016/17; lakini bajeti ya jumla ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/18 imepungua kwa **asilimia 6.89** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2016/17;


iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la **asilimia 38** katika fedha za maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2017/18, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 3.25 ya Bajeti ya Taifa, imepungua kwa **asilimia 16.13** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, **Jedwali Na. 04** linafafanua zaidi juu ya ulinganisho baina ya maeneo hayo mawili.

**Jedwali Na. 04:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais(UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa Mwaka 2017/18


| BAJETI KUU YA TAIFA 2017/2018 | | | BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2017/2018 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mgawanyo** | **Bajeti Kuu (Tsh.Milioni)** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu** | **Mgawanyo** | **Bajeti ya Wizara** | **Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara** |
| OC | 3,032,954 | 9.57 | OC | 407,136,666,674 | 49.57 |
| Deni la Taifa | 9,461,433 | 29.85 | - | - | - |
| Mishahara | 7,205,768 | 22.73 | Mishahara | 23,214,791,000 | 2.83 |
| Maendeleo | 11,999,592 | 37.85 | Maendeleo | 390,970,890,000 | 47.60 |
| **Jumla** | **31,699,748** | **100** | **Jumla** | **821,322,347,674** | **100** |

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB

Matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yanaweza kuoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-




**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18




**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

i) Serikali itoe kikamilifu mchango wake katika Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ungeweza kufanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zingetumika kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za Wafadhili. Tangu kuanza kwa mpango huu katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia **Shilingi bilioni 3.6** kati

ya **Shilingi bilioni 60.5** ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **5.9** tu.

ii) Viongozi na Watendaji waache kuingiza itikadi za kisiasa katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, kwani unaleta mgawanyiko usio na msingi kwa Wananchi na hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango;

iii) Walengwa wa Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini waelimishwe juu ya umuhimu wa kuchukua fedha zao wenyewe badala ya kutuma watu, ili waweze kunufaika na malengo mengine ya mpango ikiwa ni pamoja na kupata elimu ya afya;

iv) Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, kwenye vituo vya kutunzia Wazee nchini, kwani Wazee walioko katika vituo hivyo wanazo sifa na vigezo vya kunufaika na mpango huo;;

v) Serikali iandae utaratibu utakaowezesha Wanufaika wa Mpango wa Ruzuku kwa kaya maskini ambao wamejiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kupata huduma ya matibabu katika Zahanati binafsi. Kwa sasa Zanahati binafsi hazikubali kutoa huduma ya afya kwa walengwa hao;

vi) Serikali ihakikishe zoezi la kuhakiki na kuziondoa katika mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, kaya zisizo na sifa linatekelezwa kwa haki na kufuata taratibu ili kuepusha malalamiko ya uonevu na kutotendewa haki kutoka kwa waathirika;

vii) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa kupima na kurasimisha ardhi na biashara za Wananchi, unaotekelezwa na MKURABITA ili kutoa fursa kwa Wananchi kutumia ardhi na biashara walizonazo kujikwamua kiuchumi;

viii) Serikali ihamasishe Halmashauri kushirikiana na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi, ili kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi, na kuwezesha Wananchi kutumia Hati za Haki Miliki wanazopata kama dhamana ya mikopo kutoka taasisi za fedha;

ix) Wanufaika wa MKURABITA nchini wahamasishwe kulipia kulipia na kuchukua Hati Miliki za Kimila kwa wakati, ili kuwezesha fedha iliyotumika katika upimaji na uandaaji wa hati itumike kuendeleza zoezi hilo katika maeneo mengine;

x) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) uwezeshwe kifedha ili kutanua wigo wa shughuli zake nchini na kuongeza huduma ya mikopo kwa Vijana na Wanawake; na

xi) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kiwezeshwe kumiliki majengo kinayoyatumia katika Kampasi ya Mbeya ili kuepuka gharama za pango ambazo ni kubwa;

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkiendesha shughuli za Bunge.

Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kushiriki kikamilifu kutekeleza shughuli za Kamati. Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi ikiwa ni pamoja na siku za mwisho wa wiki. Mazingira hayo magumu hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, na badala yake walijitoa kikamilifu na kukabili majukumu yaliyokuwa mbele yao, kwa moyo na weledi wa hali ya juu wakiashiria utayari wao katika kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa, napenda niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb –Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb
6. Mhe.Esther Alexander Mahawe,Mb
7. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
8. Mhe.Halima Ali Mohamed,Mb

9. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
10. Mhe.Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
11. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
12. Mhe.Josephine Tabitha Chagula,Mb
13. Mhe.Khamis Ali Vuai,Mb
14. Mhe.Maida Hamad Abdallah,Mb
15. Mhe.Hamoud Abuu Jumaa,Mb
16. Mhe.Khalifa Mohamed Issa,Mb
17. Mhe.Hussein Ibrahim Makungu,Mb
18. Mhe.Mariam Ditopile Mzuzuri,Mb
19. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
20. Mhe.Ruth Hiyobi Mollel,Mb
21. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
22. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
23. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
24. Mhe.Zacharia Paulo Isaay,Mb
25. Mhe.Saed Ahmed Kubenea,Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Angellah Kairuki, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Utumishi, Dr. Lauren Ndumbaro kwa jinsi walivyoshiriki katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha

2016/2017, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**
18 Aprili, 2017